# *Ishara Kuu*

[Ndugu Neville anasema, "...faida ambazo Mungu ametuletea kupitia kwa huduma yako na upendo. Ambapo, kwenye wakati huu, tungetaka kuzionyesha, kwa njia ndogo, kwa kukukabidhi zawadi ndogo."—Mh.] Asante, Ndugu Neville. ["Baraka za Mungu na zikae juu yako, ndugu mpendwa."] Asante, sana sana, Ndugu Neville.

2 Na asanteni, kanisa. Kamwe sijui kilicho ndani yake. Bali ninathamini, kwa moyo wangu wote, yote ambayo mumemaanisha kwangu, na mambo ambayo mumenitendea. Na kama haikuwa ni kwa ajili yenu, kusingalikuwako na mimi. Kusingalikuwa na mtu wa kuuamini Ujumbe ambao Mungu hunipa kuhubiri, kusingekuwako na haja ya kuuhubiri. Inabidi iwe ni sisi wawili, tukifanya kazi pamoja. Kwa hiyo, ninalithamini hili sana.

3 Kanisa letu daima limekuwa, takriban, miongoni mwetu hapa, na vichekesho. Sasa, wakati nilipoingia ndani, muda mfupi tu uliopita, kwenye chumba cha nyuma, mtu fulani alinipa kifurushi, na kusema, tafadhali niende mimbarani na kumpa Ndugu Neville *hiki*. Katika kuthamini hisia zangu kwake, na ushirika wa kanisa hili, na yale ambayo amemaanisha kwetu mwaka huu, kama mchungaji katika miaka iliyopita, na matumaini na maombi kwamba ataendelea kuwa mchungaji wetu kwa miaka mingi ijayo, ishara kutoka kwa kanisa na mimi mwenyewe, Ndugu Neville.

4 [Ndugu Neville anasema, "Asante, sana, ninyi nyote. Mungu awabariki. Kweli ninathamini vitu hivyo vya fadhili na usaidizi ambavyo nimepewa kutoka kwa kila mtu katika kusanyiko hili. Na kweli mimi, asubuhi ya leo, ninajisikia kwenye kilindi cha moyo wangu ya kwamba kila wa mwisho kwetu wana shukrani sana kwa Ndugu Branham kwa yale amemaanisha kwetu, na huduma yake. Mungu na amfanikishe na kumbariki wakati akiendelea kusonga mbele kwa ajili ya Bwana mwaka huu, ndilo ombi langu aminifu. Asanteni, sana. Hakika nathamini hilo. Vema."—Mh.]

5 Watoto wadogo, vema, nafikiri hawa jamaa wadogo wanapaswa kwenda kwenye vyumba vya—vyao. [Ndugu Neville anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Na sasa kumbukeni, iweni wasichana na wavulana wazuri sana, huko nje chumbani asubuhi ya leo. Kwa kuwa, baada ya ibada, nafikiri inaonekana kana kwamba kuna kitu fulani kilichokuwa kimeachwa hapa kwa ajili yenu, kama zawadi.

6 Sasa, kwa watu wazima, kama mnavyoona idadi ye—yetu ya watoto ni—ni kubwa kweli, tunangojea kwa hamu mpaka wakati

ambapo tunaweza kuwa na kanisa jipya ambamo tunaweza kuyatenganisha hayo madarasa.

7 Dada yetu Arnold hakika ana m—mkono mzima sana; sio konzi moja, bali mkono mzima. Naye msichana wangu mdogo alikuwa akiniambia. Akasema, "Baba, ni vigumu sana kwa Dada Arnold." Akasema, "Kwa sababu, atakuwa akizungumza nasi kwa lugha ambayo tunaweza kuelewa, na halafu mtoto mchanga atafanya jambo fulani, naye itambidi kusimama na kuwasahihisha kwa hilo, unaona." Kwa hiyo inakuwa vigumu sana kwa mwanamke huyu mmoja kuwa na darasa hili lote. Kwa hiyo tunamthamini, na u—ushirikiano wake mzuri kufanya yale awezayo katika wakati huu wa mahitaji. Bwana ambariki.

8 Sasa tunatumaini, siku moja, hivi karibuni, Bwana akipenda, kuwa na maskani nzuri kubwa ambapo tutakuwa na kila namna ya vyumba kwa ajili ya madarasa ya shule ya Jumapili. Kwa watoto wachanga, walio na ubao uliopangwa wanasesere; nao wana kitalu kikubwa cha kioo, juu ya mimbara, upande *huu,* ambamo nesi aliyefunzwa atakuwako kuwahudumia hao watoto wachanga. Hakutakuwako na kukatiza ibada, hata kidogo, kutembea ama kuchapua miguu huku na huku. Jamaa hawa wadogo hawatulii, wala hawaelewi. Hawana budi kuwaelewa. Wao hawawezi kutuelewa. Na kwa hiyo, basi, mahali ambapo kila kitu kitakuwa tu jinsi ninavyoamini Bwana angeturuhusu kukifanya. Hatutakuwa na madoido, bali kanisa zuri. Tunatazamia hilo.

9 Sasa, mimi na Ndugu Neville, ndio kwanza nipate fununu, hizi zilikuwa ni suti. Sijui, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Hizo, ama kitu fulani."—Mh.] Na—nafikiri ndivyo. Sina hakika. Maana, kinaonekana kama ni kasha la suti, kwangu mimi. Hivi hujisikii vivyo hivyo kulihusu? Uh-huh. Basi ama ni suti au makabuti. Na mimi—mimi . . . Vyote viwili vinafanana, kwa hiyo i—inaonyesha hakuna upendeleo hapa. Na, kwa hiyo, mimi nina kabuti. Nami ninajua ya kwamba wao—wao . . . Si kabuti. Kwa hiyo . . . Una moja, pia, kwa hiyo lazima iwe ni suti. Na ni ninii tu . . . Tunathamini tu hili sana!

10 Nami nina hakika, ya kwamba, kama wachungaji, wachunga kondoo . . . Neno *mchungaji* linamaanisha "mchunga kondoo, mtu anayewachunga kondoo." Nina hakika ya kwamba tunawashukuru, kila mmoja wenu, kwa sababu ilikuwa—ilikuwa ni wema wenu na mawazo yenu, na pesa, zilizoifanya zawadi hii iwezekane kwetu asubuhi ya leo. Na kupitia kwa neema ya Mungu, tunajitolea wenyewe kuwa mchungaji wenu, kufanya kila tuwezacho kuwaongoza katika njia sahihi. Labda, wakati mwingine, jinsi tunavyozungumza na kadhalika, huenda ikawa ni vigumu kuelewa. Lakini tunafanya hivyo tu kama viongozi, tukijaribu kuwaongoza kwenye Mahali pale, ili kwamba, katika ule ufufuo mtatuthamini sana basi. Kwa kuwa, hatujajifikiria sisi wenyewe, katika kujiandaa wakati tunapowanenea, sio

kwa mawazo yetu wenyewe, bali kujaribu kufanya vile tu Roho Mtakatifu angetuongoza kufanya. Na hiyo ni ninii yetu... imekuwa ndiyo jitihada yetu. Nasi tungali tunajitahidi kufanya jambo lile lile, hiyo ni kweli, kwa ajili yangu mimi na mchungaji.

11 Tunashukuru kuona mwangaza wa jua. Doc, ndugu yangu, alikuwa tu akisema alituma neno kwa Ndugu Frankie Weber, huko Florida, kasema, "Siye tu anayeweza kutoka nje wakati wa Krismasi na kuosha kioo cha mbele, cha gari lake, bila koti." Alikuwa akifanya jambo lile lile, ni joto sana! Vema, mnajua Florida huchoshwa na mwangaza wa jua, ukiangalia Florida wakati wote, kwa hiyo inalibidi kuja huku Indiana na kuona jinsi kila kitu kinavyoendelea huku juu. Sivyo? Kwa hiyo, tuna furaha kwamba limetutembelea, a—angalau kwa dakika chache, asubuhi ya leo.

12 Lakini, juu ya mambo yote, tunashukuru kwa sababu ya Nuru ya Mwana wa Mungu, inayotupa upeo wa furaha ya Milele.

13 Sijui kama maskini mvulana yule mdogo, ambaye ndio kwanza aingie, angetaka kuketi pamoja na mzazi wake. Ama, kuna shule ya Jumapili huko nyuma, jamaa mdogo, kama ungetaka kwenda huko nyuma. Ndugu Taylor, naomba umwelekeze maskini jamaa huyo kwenye darasa. Hilo ni sawa. Wakati mwingine wanapenda kuwa na wenzao, mwajua. Wao, wao wana vitu shirika, wanavyotaka kuzungumzia. Na ni hivyo tu.

14 Maskini huyo msichana mwenye umri wa miaka kumi na miwili, kama ambavyo nimesema mara nyingi, kama ukimwona msichana mwenye umri wa miaka minane, tisa, kumi akikaa karibu na bibi, wakati wote, kuna kasoro fulani. Mnaona? Kuna—kuna kasoro fulani, kwa sababu kuna tofauti kubwa mno katika umri wao. Unaweza kuwazia, bibi ana kifurushi cha peremende mahali fulani, anachoweza kuingiza mkono wake. Naye maskini huyo dada ni, hayo macho makubwa ni maangavu kwa sababu ya hicho kifurushi cha peremende. Kwa sababu, kwa pamoja, wasingekuwa na kitu cha kuzungumzia, hakuna kitu ila tu angeweza kumpapasapapasa na kumbembeleza. Lakini hivyo ndivyo ilivyo, nasi tuna furaha ya kwamba ni hivyo tu.

15 Halafu basi ninatoa tamshi hilo, nililitoa wakati mmoja, juu ya kuhubiri juu ya mwana-kondoo na hua. Mnaona, wana vitu shirika. Wangeweza kuzungumzia mambo.

16 Wamasoni, Chama cha Wamasoni, wana mambo ya kuzungumzia, ndugu wa Chama cha Masoni; ndugu wa Chama cha Jamaa wa Kipekee. Wajerumani wana mambo, ya kuzungumzia, kwa Mjerumani, kuhusu nyumbani, wakati Wajerumani wanapokutana huku, mmoja ndio kwanza atoke nyumbani. Waitaliano wana mambo ya kuzungumzia.

17 Nao Wakristo wana mambo ya kuzungumzia. Hiyo ndiyo sababu tunakusanyika katika mahali kama hapa, katika

Ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu kwa sababu sisi ni raia wa Nchi ile ile. Sisi ni wasafiri na wageni hapa, kwa ulimwengu huu. Kwa hiyo tunapenda kukusanyika pamoja kwenye hizi asubuhi za sabato na nyakati za mkutano wa maombi, kukusanyika pamoja, kwa sababu tuna mambo shirika. Tunapenda kuzungumza juu ya shirika, mambo shirika, tunayoyapenda: Bwana, matendo Yake. Mtu fulani, moyoni mwao, akiwaka moto kwa kitu fulani, Bwana aliwaponya, naye anataka tu kujiwasilisha kule juu, "Angalieni yale Bwana amefanya!" Mtu fulani alipokea baraka kuu, naye anataka tu kwenda kanisani, kushiriki baraka hizi pamoja na mtu mwingine. Mnaona, hiyo ndiyo sababu tuna mambo shirika.

18 Inaonekana kwangu kwamba kusikika kwa sauti ni bora zaidi humu kanisani, asubuhi ya leo. Inaonekana kwangu. Sina hakika. Kuna kurudishwa mwangwi sana hapa ndani.

19 Lakini nina furaha sana kwa sababu ya matokeo ya uamsho wa juma lililopita. Mnaona? Haujatoa tu hamasa ya mahali hapa, bali kote, nchi mbalimbali, tumesikia kutoka kwake, kwamba Bwana alikuwa mwema. Sasa, kama kuachana tu na mambo ya kale, kutayarisha mambo, na kuingia katika Bwana, tukiwa tayari kuzipokea baraka; kama wakati huo mdogo ulifanya hivyo, ingekuwaje kama tungeendelea? Mnaona? Kwa hiyo, hebu tusiuache ufe. Endeleeni tu kuuongezea kuni, wakati wote, mpaka ishara za moshi zitaonekana kote ulimwenguni, ya kwamba Yesu Kristo yu hai, na kuna moto unaowaka mioyoni mwetu.

20 Nikiisha kujitolea upya, mimi mwenyewe, na mke wangu, na kadhalika, tumeona mambo yamebadilika sana nyumbani. Na si wenye wasiwasi kama tulivyokuwa, wasio imara na wenye mishtuko, "Hatutapata *hili,* wala hatutapata *lile.*" Tunaliendea tu kwa utulivu, na kufanya mengi zaidi.

21 Kwa hiyo, sasa, mwaka mpya unakuja. Nasi hatuamini katika kufungua kurasa mpya, tunaamini tu katika kuchoma ya kale. Kwa hiyo endelea tu kujiweka wakfu kwa Mungu kote katika mwaka ujao, hatujui yale Bwana atakayotufanyia.

22 Lakini tunashukuru kwa ajili ya kila mmoja wenu. Ninamshukuru Mungu sana kwa ajili ya kila mshiriki wa Mwili wa Kristo, kila mahali. Na katika awamu zote mbalimbali za imani, haidhuru wanaweza kutofautiana nami kiasi gani, ningali ninashukuru ya kwamba mtu fulani. . .Hata kama ningewazia wangekuwa makosani kidogo, katika Maandiko, lakini hata hivyo wakijaribu kutetea kwa bidii kile wanachoamini. Hakika niko tayari kuvumiliana na hao ndugu, nao wanivumilie katika makosa yangu na kadhalika, kwa sababu hakuna mmoja wetu aliye mkamilifu.

23 Lakini katika ule Ujumbe hivi majuzi jioni, wakati nilipozungumza juu ya Mungu kujigawa Mwenyewe katika

Pentekoste, katika njia panda ya wakati, ama kwenye kongamano ambako ilibidi uamuzi ufanywe, "Hili Kanisa jipya la Kikristo litakuwa ni la aina gani?" Hiyo ndiyo sababu ya kufanya hilo kongamano. Nasi tunaona ya kwamba katika Kitabu cha Matendo, mlango wa pili, tunaona aina ya kanisa lililokubalika; ni Kanisa la aina gani, kile hilo Kanisa lingekuwa, jinsi kanisa lingetenda wakati lilipompokea Kristo. Ninapenda jambo hilo. Nami ninashindania kwa bidii hilo Kanisa ambalo lilianzishwa kwenye Siku ya Pentekoste mara moja tu. Sasa, lilikuwa la kipekee wakati huo, ni la kipekee sasa. Nalo litakuwa, maadamu kuna dhambi duniani, na vita vya kupiganwa, litakuwa la kipekee kwa maadui wetu, lakini hata hivyo ni mambo ya thamani ya Mungu ambayo tunashindania kwa bidii kwamba Mungu atatufanyia.

24 Sasa, matangazo, nadhani Ndugu Neville tayari ameyatangaza.

25 Basi nikiwa nyumbani juma hili, kuomba na kuutafuta uso wa Bwana. Kwa kuwa, katika mwaka huu ujao, kwa msaada wa Mungu, endapo tu atanisaidia, ninataka kupiga vita kwa nguvu zaidi kuliko nilivyopata kufanya maishani mwangu mwote. Na labda sehemu kubwa sana ya mwaka huu itatumika kwenye huduma za nchi za ng'ambo, na Haiti, na visiwani, na Marekani ya Kusini, na Afrika, na Asia, na India, na—na huko juu katika Scandinavia. Na yote hayo yataamuliwa juma hili, Bwana akiruhusu. Kwa hiyo ninapojisikia kuongozwa kufanya jambo lolote ama kwenda popote, Bwana amenituma kufanya hivyo.

26 Basi ninaposhuka kwenye ndege, ardhini, na inaonekana kama huyu hapa mmoja anakuja, na kusema, "Loo, dhehebu *hili* moja lilijiondoa, *hili* lilifanya hivi, ama *hili* lilifanya makosa, ama tusingeweza kufanya *hili,* ama viongozi wanasema hatuwezi kufanya mkutano."

27 Ndipo ningependa kusimama, "Lakini nimekuja katika Jina la Bwana." Nami ninajua huyo ni ibilisi, basi. Mnaona, sivyo, "Hivi nilikosea?" Ninaongozwa. Ndipo unaweza kusimama kwa juhudi kubwa, na kupiga vita.

28 Sasa, kabla hatujakifungua Kitabu, ama kumwomba Mungu akifungue tunapokisoma, ningetaka kusema sababu ya mimi kuuleta Ujumbe huu kwa kanisa asubuhi ya leo. Ni Ujumbe wangu wa Krismasi kwa kanisa. Ni ninii. . .kama Roho Mtakatifu atanisaidia kuwasilisha kile ninachoamini juu yake. Sasa, haidhuru limeandikwa vizuri jinsi gani katika Maandiko, na kadiri mtu anavyolielewa, bado hawana budi kumtegemea Roho Mtakatifu kuuleta kwa watu. Na ni baada tu ya Krismasi, wakati mmesikia kila namna ya hadithi za Krismasi na—na matangazo, na kadhalika, ya jumbe za Krismasi. Huu utakuwa kidogo ni wa kipekee, kwa ajili ya hadithi ya Krismasi, lakini hata hivyo Mungu ameuweka moyoni mwangu.

29 Na sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu, katika Uwepo Wake na vivuli vya haki Yake, tuombe rehema.

30 Ee Mungu, Mwokozi wetu mbarikiwa na Baba, tunakikaribia kiti Chako cha rehema. Katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao, tunajikabidhi kwa unyenyekevu asubuhi ya leo, kukutolea Wewe maombi yetu na shukrani zetu, kwa yote ambayo umetufanyia. Katika juma hili lililopita, hasa, jinsi ambavyo mioyo imekuwa na njaa, nao watu wamefunga, na Roho Mtakatifu amewabariki, amefanya mambo makuu katikati yetu! Wagonjwa wameponywa. Na Mungu ametambulikana, kwamba Yeye yu hai, Naye anawapenda watu Wake.

31 Na kwamba hayo Maneno yangali ni kweli, ya nabii, hapo aliponena Maneno ya Bwana Mungu, wakati aliposema, "Kama watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja, na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni." Maneno hayo ni ya kweli tu kama ile siku yaliponenwa kwanza. Tuliona hilo kuwa hivyo, Bwana. Sasa tusamehe, tunaomba, dhambi zetu zote, kutokuamini kwetu kwote, ambako ni dhambi.

32 Nasi tungeomba, Bwana, ya kwamba Wewe utaturejeshea imani ile ambayo wakati mmoja ililiendeleza Kanisa lile la kwanza. Hatuombi tupate maisha ya starehe, bali tunaomba tu rehema ya Mungu, na kwa Uwepo Wake, na baraka Zake kuambatana nasi. Kama ni kwenye huduma hii ama huduma ng'ambo ya bahari, kama ni kwenye anasa, ama maisha ya starehe, ama ni katika uwanja wa vita, haidhuru ni wapi, Bwana, mapenzi Yako yaliyo madogo sana ndiyo shauku yetu kuu ya kukutumikia. Lifanye tu dhahiri kwetu, Ee Bwana, hata hatutapotea njia, kwa kuwa tunatembea katika ulimwengu wenye giza na uliopofuka, miongoni mwa watu wenye dhambi waliopofushwa. Kwa hiyo, isafishe njia yetu, Baba, na utuongoze utakavyo, kondoo wa malisho Yako.

33 Jalia Mchungaji wa kundi kwa utamu na unyenyekevu awaongoze watu Wake, tunapokungojea asubuhi ya leo kwa ajili ya Ujumbe wa asubuhi ya leo. Jalia Roho Mtakatifu anene dhahiri kwa kila moyo na tupate mtazamo wa mara moja wa yale nabii alikuwa akizungumzia, na katika hilo, basi, tupate baraka tukufu za Uwepo wa Mungu, kuthibitisha kila Neno. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mwanao, Mwokozi wetu. Amina.

34 Ningeliomba kusanyiko letu asubuhi ya leo, wale walio na Biblia, kama wangetaka kusoma pamoja nami, Maandiko, ama kunifuata ninapoyasoma, kama mtafungua kwenye Kitabu cha Isaya. Nabii Isaya, na mlango wa 7, ningetaka kusoma kutoka kwenye sehemu ya Maandiko haya. Katika Isaya, mlango wa 7, tutaanza na mazungumzo ya Mungu kwa Ahazi, kwenye kifungu cha 10.

*Tena Bwana akasema na Ahazi, akinena,*

*Jitakie ishara ya* B*WANA* *Mungu wako; itake katika mahali palipo chini sana, au katika mahali palipo* juu *sana.*

*Lakini Ahazi akasema, Sitaitaka wala sitamjaribu* B*WANA*.

*Naye akasema, Sikilizeni . . . Enyi nyumba ya Daudi;* Je, ni *neno dogo kwenu kuwachosha wanadamu, lakini je, mnataka kumchosha Mungu wangu pia?*

*Kwa hiyo Bwana Mwenyewe atawapa ishara; Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye . . . atamwita jina lake Imanueli.*

*Siagi na asali atakula, apate kujua kuyakataa . . . mabaya, na kucha- . . . kuyachagua . . . mema.*

*Kwa kuwa kabla mtoto huyo hajajua kuyakataa . . . mabaya,* au *kuyachagua . . . mema, nchi ile ambayo wewe unaichukia itaachwa na wafalme . . . wawili.*

35 Kama napaswa kusema somo kutoka kwa hili, kutoa muktadha, ningetaka kutumia neno: *Ishara Kuu*.

36 Tunapokuwa na usiku wenye giza sana, na inaonekana kwamba katika . . . wakati mwingine kunaonekana giza sana katika usiku huu hata hatuwezi hata kuiona mikono yetu mbele zetu, ni kwenye wakati huo ambapo ile radi iliyogawanyika ni angavu sana. Inatumwa kwetu kuonyesha ya kwamba kunaweza kuwa na nuru gizani.

37 Hii ilikuwa ni kwenye wakati wa utawala wa Ahazi, mfalme mwovu. Na kama mliangalia, Bwa—Bwana kamwe hakuuelekeza huo ujumbe kwa Ahazi, bali kwa nyumba ya Daudi. "Sikilizeni, Enyi nyumba ya Daudi! Hii itakuwa ndiyo ishara." Kwa sababu, walikuwa vitani, ndugu dhidi ya ndugu, na ilionekana kuwa saa yenye giza kuliko zote kwenye safari ya Israeli na kusafiri kwao. Lakini Mungu akatangaza, kupitia kwa nabii, ishara ya Milele. Sasa, ishara mara nyingi . . .

38 Watu wanazo ishara. Nasi tunaishi katika ulimwengu uliojaa ishara. Mwanadamu amejaribu kufanikisha ishara fulani. Mwanadamu amejaribu, kupitia kwenye utafiti wake wa kisayansi, kwa ufanisi wake mwenyewe, kufanya ishara ambayo ingekuwa ni nzuri sana, ama kumbukumbu ya akili zake, juu ya jinsi alivyo mkuu, ama jinsi alivyo mwanzilishi. Amefanya hivyo kwa miaka mingi.

39 Kwa mfano, wakati mabingwa wa baharini wa ulimwengu, chini ya miaka mia moja iliyopita, walipoamua kwamba walikuwa ni werevu sana hata wangeweza kuupa ulimwengu i—ishara ya ustadi wao hodari, ya kwamba wangeweza kujijengea meli ambayo hakuwezi kuwa na wimbi kubwa kutosha kuizamisha. Nao wakaiita meli hii Titaniki. Ilikuwa ni kumbukumbu ya kudumu kwa ulimwengu, kwamba ule

ufundi mkuu wa kujenga meli ulikuwa umefikia ukamilifu, kwamba wangeweza kuuonyesha ulimwengu ya kwamba meli hii isingeweza kuzama.

40 Kwa hiyo, pamoja na usalama wote juu ya akili za hao wajenzi, na hotuba na mazungumzo yao, na mathibitisho ya kisayansi ya kwamba meli hii isingeweza kuzama! Ndipo wakati mambo yanapowasilishwa kwa watu namna hiyo, wana—wanaonekana kushawishika kwamba kila kitu ni shwari, maadamu utafiti wa kisayansi unasema kwamba ni sawa.

41 Kwa hiyo walikuwa wakiivuka bahari katika meli hii, kwenye safari yake, wakijisikia salama sana kwamba hakuna kitu kingaliweza kuwadhuru, wakafanya karamu kubwa ya ulevi. Basi wanawake wote na wanaume melini, ama, labda wengi wao, huenda nikasema, wakalewa; hata, wanasema, hata nahodha na rubani, na wote. Ndipo bendi zikaanza kufanya shamrashamra za mu—muziki wa jazi, ambao ulikuwa ndio kivutio kikuu cha siku hizo, kama tulivyo na roki siku hizi. Kwa sababu, walikuwa salama, walikuwa kwenye meli ambayo wanadamu walikuwa wameupa ulimwengu ishara ya akili zao, ya kwamba, "Meli hii ingeweza kukabiliana na kila wimbi ama bahari yoyote."

42 Walipokuwa katika shamrashamra hizi za ulevi, ikaelekea kwenye ukungu. Ndipo mmoja wa manahodha akasema, kwamba, "Inatupasa kuzichunguza injini." Lakini mwenye mamlaka yote akasema, "Iendeshe, 'Mbele moja kwa moja!' hatuna budi kuwa bandarini kwa ajili ya wito fulani." Wakati ilipokuwa ikiingia kwenye ukungu, kana kwamba ilikuwa ndiyo bingwa wa hali ya mambo, kwa ghafla, ikagonga korongo la barafu, na hiyo ikazama chini ya maji.

43 Nasi tunaambiwa na yule mshairi aliyeuandika ule wimbo, "Mungu, kwa mkono Wake wenye nguvu, anaonyesha ulimwengu huu hauwezi kusimama."

44 Ufanisi wao mkuu uliingia chini ya bahari, pamoja na mamia mara mamia ya walevi melini. Haitafaa kitu kamwe.

45 Ilikuwa ni hayati Adolf Hitler aliyewapa Wajerumani ishara ya kwamba yeye alikuwa na kipaji, alijua yote kuhusu maisha ya kijeshi. Basi, pasipo kumpunguzia sifa, alijua mengi kuyahusu. Lakini aliwahakikishia Wajerumani, kwa kujenga kile tunachoita Ngome ya Maginoti, ama Ngome ya Siegfried, ambamo alimwaga mabilioni ya tani za zege na chuma kigumu pamoja. Akaonyesha matumaini yake kwake, hata akayahamisha makao yake makuu kwenye uwanja wa vita, ambako mikahawa na mahali pa biashara paliendelea chini ya ardhi, ambamo walikuwa na mabilioni ya tani za chuma kigumu na saruji. Haidhuru viliendaje, Ujerumani ilikuwa imeimarishwa. Ilikuwa ni alama ya usalama. Lakini makombora ya kisasa yaliilipua hadi Umilele, na Hitler pamoja nayo.

46 Ilikuwa ni Nimrodi, siku moja, aliyesema kwamba angejenga mnara ambao ungewaleta watu wake, angeweza kuonyesha yale aliyoweza kufanikisha kwa akili yake. Naye alikuwa ajenge mnara ambao ungeyapita mawingu, ambao, kama ghadhabu ya Mungu ikija wakati wowote, yeye angeweza kumshinda akili. Pamoja na utafiti wake wa kisayansi, angeweza kuweka miamba na mawe hivi kwamba angeweza kuwapeleka watu kwenye usalama, kwa akili zake. Lakini uliangamizwa kabisa, kwa machafuko ya lugha, wala hata wasingeweza kuumalizia huo mnara.

47 Ilikuwa ni Nebkadreza aliyezijenga kuta za Babeli, kisha akazijivunia. Kubwa sana, hata, farasi sita na magari ya farasi wangeweza kukimbia kuzizunguka hizo kuta. Malango yake yalikuwa ni makubwa sana, hata watu waliyatolea jasho maishani mwao, wakipiga shaba kufanya malango ambayo yalikuwa na uzito wa mamia ya tani; katika hilo jiji kuu, ilihitaji makundi ya watu kuyafungua. Hakuna mtu angaliweza kumgusa Nebkadreza. Lakini usiku mmoja, katika shamrashamra za ulevi, wakifikiria kwamba walikuwa salama nyuma ya kuta zao za kisayansi, pamoja na zana za vita za siku zao, yalitokea maandishi ya Mkono ukutani. Nao ukaisha.

48 Loo, jinsi mwanadamu amejaribu kumpeleka mwanadamu kwenye usalama, kujisukuma hadi kwenye usalama, kwa ishara zake mwenyewe za ufanisi. Inaonekana kana kwamba, kwa sababu kwamba wanadamu wanatafuta ishara, hapana shaka kuna sababu yake; kitu fulani ndani ya mwanadamu ambacho kingetamani kupata sababu ama ishara, kutoka mahali fulani, kwamba angeweza kuwa salama.

49 Ndipo Mungu akanena, kasema, "Nitawapa ishara ya milele. Nitalipa kanisa ishara ya milele." Haikuwa iwe ukuta mkubwa wala mnara. Yeye alisema, "Bikira atachukua mimba, na kuzaa Mwana, na atamwita Jina Lake 'Imanueli.' Hiyo itakuwa ni ishara ya Milele ya Mungu." Jinsi ilivyo rahisi! Jinsi ilivyo duni!

50 Je, unaelewa ya kwamba ni mambo madogo unayoyapita na kuyapuuza, yanayomaanisha mengi sana kwa Mungu? Je, kanisa linaweza kupata hilo asubuhi ya leo? Katika ufanisi wetu kama dhehebu, na mijengo yake mikuu na vipeo vyake, tunapuuza vile vitu vidogo vinavyomaanisha mengi sana kwa Mungu na mengi sana kwa kikomo chetu cha Milele. Tunavipuuza vitu hivyo.

51 Mungu akisema, ya kwamba, "Nitawapa ishara ya Milele. Bikira atachukua mimba, na kuzaa mtoto."

52 Mbona, mbona mtoto mchanga, kwa nini iwe ni m—mtoto mchanga? Ati Muumba Mwenyewe hana budi kuja na kuishi katika kiumbe Chake, kuwa ishara kwa mwanadamu? Kwa nini iwe mtoto mchanga? Kwa nini Yeye asingalisema, "Nitajenga ngazi kuu, nanyi nyote. . .kama ile ndoto ya Yakobo. Ama, nitashusha kutoka Mbinguni, kutoka kwenye ushoroba wa

Mbinguni, kamba, na kuwapa nguvu, ili kwamba, mkijifunga kwake, nitawainua juu”?

53 Lakini, Yeye alikuja kwa urahisi sana. Kisha kasema, “Mtoto mchanga atazaliwa. Hiyo itakuwa ni ishara. Si kwamba tu itakuwa ni ishara, bali itakuwa ni ishara kuu.” Mtoto mchanga! Mbona, akili ya sayansi ingecheka machoni pa wazo kama hilo. Lakini, kwa Mungu, ilikuwa ni ishara kuu. “Bikira atachukua mimba, naye mtoto huyu ataitwa *Imanueli*, ambalo tafsiri yake itakuwa, ‘Mungu pamoja nasi.’” Hiyo ndiyo ishara kuu.

54 Mungu wa Mbinguni, akiishi pamoja na watu, ndiyo ishara kuu. Ingekuwa si ishara kwa ajili ya siku hiyo pekee, bali kwa ajili ya siku hii na kwa siku zote, kwamba Mungu anaishi pamoja na watu Wake. Imanueli, Mungu pamoja nasi, hii ndiyo ishara kuu. Hii ndiyo ishara ya Milele, ishara isiyo na mwisho, aliyoitoa Mungu.

55 Basi kwa nini Yeye akafanyika mavumbi, mavumbi yenyewe ya uumbaji Wake Mwenyewe? Muumba alifanyika hayo, mavumbi ya uumbaji Wake.

56 Mwanadamu akijaribu kufanya kitu kikubwa mno. Lakini, wakati Mungu alipotoa ishara, ilikuwa ni kitu kidogo. Mwanadamu hujaribu kushughulikia mambo makubwa. Mungu hushughulikia mambo madogo. Mwanadamu hujaribu kusema, “Kwa sababu kila mtu huenda *hivi*, hebu tufanye kama wafanyavyo katika Hollywood.” Mungu anataka uchache. Anataka ku—kupuuza mambo yote makubwa, apate kupokea lile dogo.

57 “Mtoto atazaliwa, mtoto Imanueli atazaliwa.” Mungu wa viumbe akawa sehemu ya viumbe Vyake Mwenyewe. Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Yule aliyeumba mavumbi na miti, na mambo yote yaliyopo, alifanyika mmoja wao. Hiyo itakuwa ishara, Yeye atapitia njia hiyo kwa mwanadamu.

58 Sasa, Yeye angeweza kuja njia nyingine. Yeye angalikuja kwa njia ya mwingine, kwa—kwa njia zingine alizo nazo Yeye za kuja.

59 Lakini akachagua kuja kwa njia hii, kutoa ishara, ishara kuu. “Bikira atachukua mimba, na kuzaa Mwana, nao watamwita ‘Imanueli.’” Sasa, ilikuwa ni kwa ajili ya nini? Sababu gani?

60 Kwa nini hakuchagua kuwa Malaika? Angalifanya hivyo. Angeweza kuja m—mtu mzima kabisa. Angaliweza kuja na gwaride kamili kutoka Mbinguni, pamoja na Malaika na Wenye uhai wote wa Mbinguni; waweke chini kutoka ushoroba wa Mbinguni, ile ngazi ya dhahabu, Naye angeweza kushuka pamoja na bendi ya Malaika. Angalifanya hivyo.

61 Lakini Yeye alisema, “Nitawapa ishara, ishara kuu, ishara ya milele. Bikira atachukua mimba, na kumzaa mtoto.”

62 Na wakati ilipombidi kuchagua mahali ambapo mtoto huyu angezaliwa. Angeweza kushuka kwenye hiyo ngazi, pamoja na gwaride kamili la Mbinguni. Angeweza kushuka kutoka Mbinguni kama Malaika, ama ashuke kama mtu mzima kabisa. Lakini Yeye, pia, angeweza kuja katika ikulu ya mfalme.

63 Bali akasema, "Nitawapa ishara." Nayo ishara hiyo waliambiwa wachungaji, "Mtamkuta horini, amevikwa nguo za kitoto." Hiyo ndiyo ishara kuu, amezaliwa juu ya lundo la samadi, na harufu mbaya ya hilo zizi, bila hata na nguo za kumvika, Imanueli. Ibilisi anataka kufanya mambo makubwa na maangavu. Mungu huyanyenyekeza mambo. Ishara kuu, "Mtamkuta mtoto amevikwa nguo za kitoto, amelazwa horini. Hii itakuwa ishara, ishara kuu." Wakati alipokuwa duniani, Yeye alikuwa maskini sana. Jinsi tunavyozungumza juu ya wakati mgumu? Ni nani Mtoto huyu? Ni Yehova!

64 Yehova Mungu alifanyika mwanadamu, akawa wa ukoo wetu, akajibadilisha Mwenyewe kutoka kwa Mungu, akawa mwanadamu. Hiyo hapo ishara. Akafanyika . . . Yeye alikuwa ni Mungu, kisha akafanyika mwanadamu; sio tajiri, bali maskini. Hii ndiyo ishara kuu. "Mmejitakia ishara," kasema Mungu, "Nitawapa ishara, ishara ya milele."

65 Angalikuja vinginevyo, kama nilivyosema, lakini, mtoto mchanga, kwa nini Yeye akafanyika mtoto mchanga? Wakati maskini kinywa hicho cha kwanza, kisicho na meno, kilipofunguka horini, kwenye hilo hori la kwanza . . . asubuhi ya kwanza ya Krismasi, katika maskini hori Lake la zizini, na yowe dogo la kwanza lililotoka kwenye sauti Yake, huyo alikuwa ni Mungu akilia. Yehova akilia, mwanadamu; aliyetoka kwa Mungu, naye alikuwa ni mwanadamu, kwa kila hali, mwanadamu. Alikuja ulimwenguni bila chochote, bali angali ni mwanadamu. Alikuwa akijaribu kufanya nini? Alikuwa akikusudia nini?

66 Alilia kama mtoto mchanga, katika hori. Akacheza kama mvulana, mtaani. Alifanya kazi kwa bidii kama mwanadamu, lakini hata hivyo alikuwa ni Imanueli. Hii ndiyo ishara kuu. Mungu akiishi katika kiumbe alichokiumba. Ishara kuu, "Itakuwa ni ishara kwenu."

67 Alikuwa maskini sana, wakati alipokuja duniani, alipitia kwenye tumbo la uzazi lililoazimwa, tumbo la uzazi la mwanamke lililoazimwa. Kisha ilimbidi kuazima kaburi, apate kuzikwa mle. Mungu! "Bikira atachukua mimba, pasipo na kuingiliwa kati na kujuana kimwili." Yehova aliazima tumbo la uzazi la Mariamu, mwanamke, apate kufanya jukumu ambapo Yeye angetoa ishara ya milele. Naye alikuwa maskini sana, duniani, baada ya miaka thelathini na mitatu na nusu, ya huduma, ilimbidi kuazima kaburi azikwe humo. Mnaweza

kuwazia? Nena kuhusu kuzaliwa pasipo na dhambi ya asili, unamaanisha nini, kwa vyovyote vile?

68 Hivi hamwezi kuona ile ishara halisi? Ni Yehova akifanyika mmoja wetu. Yehova Mungu duniani, kama mkimbizi, msafiri katika nchi aliyoumba Yeye; amekataliwa, akasukumwa, na kuchekwa, na kudhihakiwa; Jiwe la kujikwaa kwa asiyeamini, Mwamba wa chukizo; ibilisi, kwa ulimwengu wa kidini. Lakini ishara ya Milele kwa mwaminio, "Mungu pamoja nasi," ishara kuu. Mnaliona? Mungu akidhihirishwa, Mungu akijiwasilisha Mwenyewe kwa ulimwengu, kama mkimbizi. Angeweza kuja kwa njia nyingine, bali alichagua kuja namna hii.

Sikilizeni Hili. Msilikose.

69 Nafikiri kwamba Mungu aliwazia niani Mwake, ingemvutia mwanadamu. Inavutia, kwa mwaminio. Inavutia wakati Mungu wetu anapofanyika mmoja wetu. Lakini, kwa walio baridi, waovu, jiwe la kujikwaa. "Nitawapa ishara, bikira atachukua mimba. Imanueli atakuwa pamoja nanyi." Mungu aliwazia lingeivutia jamii ya binadamu, kwamba Mungu wetu angekuwa mmoja wetu, kwamba angejibadilisha Mwenyewe na kufanyika mavumbi yetu, kwamba angefanyika wa ukoo wetu, ukoo wa kibinadamu; Muumba Yule aliyeumba vitu vyote.

Na, tena, ilitimiza unabii. Manabii walikuwa wameliona.

70 Na jambo lingine, "Neno lilifanyika mavumbi, mwili, na kukaa miongoni mwetu." Yehova, Neno lilifanyika mwanadamu, likafanyika mavumbi na kufanya makao pamoja nasi. Ishara ya *Milele*, "kamwe haitaisha." Loo, tunapoiwazia, ishara ya Milele, ishara kuu za ishara zote, Mungu akifanyika mmoja wetu.

71 Halafu, tena, Yeye hana budi kuwa ni uzao wa Ibrahimu. Ibrahimu, bila shaka, alikuwa ni uzao wa Hawa. Hawa... "Alikuwa ni Uzao wa mwanamke utakaokiponda kichwa cha nyoka." Lakini, Ibrahimu, kama mnaweza kulishika, alikuwa na imani katika Mungu, ambayo iliiunganisha Roho ya Mungu pamoja na mwili wa mwanadamu. Hapo ndipo imani inapokuja. Hapo ndiyo sababu Yeye angekuwa Uzao wa Ibrahimu, sio mwili wote, bali kule kuunganishwa kwa Roho na mwili pamoja. Mungu, akijifanya Mwenyewe... akirarua, aking'oa uovu wote, akiutiisha mwili, mavumbi aliyoumba Yeye, na kuishi pamoja nanyi kama mwe—mwenzi.

72 Jambo lingine, Yeye hakutia najisi wala kwenda kinyume cha yoyote ya sheria Zake. Hawezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, "Bikira. Nitawapa ishara." Sio Titaniki, sio U.N., bali, "Nitawapa ishara ya usalama. Bikira atachukua mimba, naye atazaa Mwana, na kumwita 'Imanueli.'" Hiyo ndiyo ishara. Naam.

73 Mnaona, katika sheria za Mungu za ukombozi, kama ilivyokuwa kwa Boazi na Naomi, ilibidi awe jamaa wa karibu. Na njia pekee ambayo mwanadamu angeweza kukombolewa, ilibidi Mungu afanyike jamaa, wa karibu. Ninawatakeni mlione.

Yeye kamwe hakufanyika wa ukoo, kwa jumla, kwa matajiri, kwa wenye nguvu. Lakini Yeye alizaliwa katika zizi, akafunikwa nguo za kitoto; si kwa mtu mzima, bali kwa mtoto. Yeye alikuwa ni Mungu juu ya uumbaji. Alichagua kufanya hivyo, sio kuja akiwa mtu mzima kabisa. Alikuja aweze kupatwa na hisia za watoto wachanga. Alikuja aweze kupitia majaribu ya matineja. Apate kwenda, aweze kutaabika taabu na mitego ya ibilisi, kama mwanadamu, na kufanya njia kwa ajili ya watu wa umri wote, wa umri wote na wa matabaka yote: maskini, tajiri, wote. Alifanyika maskini, ili kwamba, kupitia umaskini Wake, tupate kuwa matajiri na warithi pamoja Naye katika ule Ufalme. Ishara ingetolewa, akijibadilisha Mwenyewe, akijifanya Mwenyewe kitu fulani tofauti na kile alichokuwa; sasa ishara kuu, akilia kama mtoto mchanga, akicheza kama mvulana, akitaabika kama mwanamume, bali ilikuwa ni Mungu akiishi hatua zote za maisha kama tufanyavyo sisi.

74 Mnajua, Mungu ametoa ishara nyingi kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Alitoa ishara kwa ulimwengu ulioitangulia ile gharika, kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, Mungu wa hukumu. Aliwazamisha watu katika siku za Nuhu, na kuwafanya wenye haki waelee katika safina; ishara ya kwamba alikuwa ni mwenye haki, na hukumu ilikuwa ni ya hakika. Hiyo ni ishara, ya kwamba kila mwenye dhambi asiyetubu ataangamia katika hukumu, ya kwamba wenye haki wataokolewa kwa rehema ya Mungu.

75 Alitoa ishara nyingine kwenye kichaka kilichowaka moto. Ilikuwa ni nini wakati alipomshika nabii Wake mtoro, "Nimesikia vilio vya watu Wangu, nami nimekumbuka agano Langu"? Yeye alitoa ishara nyingine pale, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu anayetimiza agano, ya kwamba alikumbuka kila kitu alichosema, kila ahadi aliyotoa. Akatoa ishara kwenye kichaka kilichowaka moto, "Nami nimeshuka kuja kuwakomboa."

76 Mwangalie Mungu katika njia Zake za kazi. Wakati alipoumba Mbingu na nchi, Yeye aliwakusanya Malaika pamoja, ndipo akasema, "Hebu sisi." Kila mahali katika Maandiko ambapo alifanya lolote, zaidi sana, "Sio Mimi, bali Baba Yangu."

77 Lakini ilipofikia mpango wa ukombozi, Yeye alikuja peke yake. Hakuna mtu aliyekuwa pamoja Naye. Yeye Ndiye wa pekee angaliweza kuja. Malaika asingeweza kufanya hivyo. Mtu mwingine, aliyeitwa Mwanawe, asingeweza kufanya hivyo. Mmoja aliyeitwa kitu kingine, bikira mtakatifu, ama mama mtakatifu, ama—ama mtakatifu fulani, asingeweza kufanya hivyo. Ilimbidi Mungu kuja! "Nami nitawapa ishara. Bikira atachukua mimba; naye mwana atazaliwa, Naye atakuwa ni Imanueli, Mungu pamoja nasi," ishara kuu. Mungu katika watu Wake. Mungu pamoja na watu Wake. Mungu akafanyika watu Wake. Mungu na mwanadamu wakawa mmoja. Ishara! Jiwe

la kujikwaa kwa ulimwengu, bali tumaini lenye baraka kwa mwaminio. Ishara itakayonenwa vibaya.

78 Yeye alikuwa na wakati mwingine ambapo alithibitisha. Alithibitisha kwenye ile gharika ya kwamba alikuwa Mungu wa hukumu, na Mungu wa rehema kwa wale wanaotii Amri Zake.

79 Alionyesha kwenye kichaka kilichowaka moto, kwa ishara, ya kwamba Yeye angetimiza kila ahadi aliyotoa.

80 Na kwenye Bahari ya Shamu, alionyesha ya kwamba angefanya njia kwa ajili ya wale waliokuwa wakijaribu kufanya mema na kuzifuata Amri Zake. Haidhuru ni kitu gani kinachozuia, Mungu alithibitisha kwenye Bahari ya Shamu, na kutoa ishara, ya kwamba angeweza kuifungua bahari. Katika kila jaribio, Yeye atafanya njia ya kuepukia. Wasema, "Mama haliamini. Baba haliamini. Kanisa haliliamini." Sijali ni nani asiyeliamini. Ikiwa wewe unaliamini, Mungu atafanya njia ya kuepukia. Alitoa ishara kwamba atafanya hivyo. Walikuwa njiani, moja kwa moja wakielekea nchi ya ahadi, ambako Mungu aliwaahidi. Ndipo Bahari ya Shamu ikawafungia nje, nao wakaingia katika matatizo. Hawakujua la kufanya. Mungu alionyesha ya kwamba Yeye angefanya njia ya kuepukia katika kila jaribio, kila jaribu. Ati huwezi kuacha kuvuta sigara? Mchukue Mungu wakati mmoja. Ati huwezi kuacha kusema uongo, huwezi kuacha kuiba, huwezi kuacha kuwa na hasira? Mchukue Mungu pamoja nawe wakati mmoja. Kama hujisikii kwenda kanisani, wala huwezi kufikia popote; mchukue Mungu pamoja nawe wakati mmoja, ichukue ahadi Yake. Yeye alithibitisha, kwenye Bahari ya Shamu, ya kwamba atafanya njia ya kuepukia. Mungu ametoa ishara nyingi.

81 Usiku huo wakati alipowaambia wachungaji, "Shukeni mwende Bethlehemu, kwa kuwa leo hii amezaliwa Kristo Mwokozi. Kristo, Mungu aliyetiwa mafuta, leo hii amezaliwa na mwanamke." Mungu!

82 Sio kumfanya huyo mwanamke mungu, sasa. Yeye aliazima tu tumbo la uzazi la huyo mwanamke, kama vile anavyoazima mwili *huu* kuhubiria Injili. Kama vile anavyoazima mwili wako, kufanya kazi anayotaka kufanya kupitia kwako, kwa sababu Yeye angali ni Imanueli, ishara, Mungu pamoja na watu Wake. Mungu akiishi miongoni mwa watu Wake, ishara kuu, ya milele. Kamwe haiwezi kushindwa. Daima itakuwa ni ishara.

83 Unazungumza kuhusu ishara hizi, na hii je? Kabla hujaweza kupata ishara nyingine yoyote, ishara ya kunena kwa lugha, ishara ya kutabiri, ishara ya yoyote ya kimbinguni, itakubidi kurudi kwenye ile ishara ya asili, ya Milele na ishara ya daima. Kuwa sawa, kwanza kabisa, na juu ya msingi huo, ambao ni Mwamba kote katika nyakati, wala hakuna kitu kitakachougusa kamwe. Malango ya Kuzimu yataipinga, bali

hayawezi kushinda. Pata ishara hiyo, “Bikira atachukua mimba, na kuzaa Mwana.”

84 Naye akawaambia hawa wachungaji, “Hivi ndivyo mtakavyompata. Atakuwa horini, katika kibanda, amefunikwa nguo za kitoto. Ndipo mtakapomtazama, aminini, kwa kuwa Yeye ni Mungu miongoni mwetu.”

85 Ishara hiyo haikuwa tu kwa wachungaji. Lakini ilitolewa kwa ulimwengu wote, kumtazama na kuona kwamba Yeye ni nani. Ni Mungu pamoja nasi, Imanueli.

86 Wakati alipokuwa hapa duniani, alithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Alithibitisha ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake, kwa sababu ishara za Mungu zilifuatana Naye. Alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama ninazitenda hizo kazi za Baba Yangu, msiponiamini Mimi, amimini hizo kazi, ile ishara.” Imanueli! “Mimi na Baba Yangu ni mmoja. Baba Yangu alinituma. Na kama Yeye anavyonituma, Mimi nami nawatuma. Baba, aliyenituma, yuko pamoja na Mimi. Yeye yuko ndani Yangu na kufanya kazi zake Mwenyewe. Ni Mungu katika mwili.”

87 Hivi Lutu hakupata kionjo cha hilo kabla ya yale maangamizi? Wakati, yeye alipomwona Mungu amedhihirishwa katika mwili, akila ndama, akinywa maziwa ya ng’ombe, na kula mkate kutoka mekoni, na kusimama huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, na pamoja na kiwakilishi nafsi “Mimi.” “Mimi, kwa kuwa Ibrahimu ndiye mrithi wa ulimwengu, Mimi . . . ” Kwa maneno mengine, “Nitamfahamisha.”

88 Ilikuwa ni Nani? Kisha akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Lilimshtusha. Mungu, katika onyesho la kimbele la Kristo, kufanyika mwili.

Akasema, “Yuko hemani, nyuma Yako.”

Sara akacheka. Na Yeye akasema, “Kwa nini Sara akacheka?”

89 Wakati Imanueli alipopitia kwenye tumbo la uzazi la mwanamke, badala ya kutokea kama thiofania, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

90 Wakati alipokuwa duniani, hao mitume walitoka wakaenda pamoja na Injili, hata Malaika wakaangalia kwenye uzio wa ngazi za Mbinguni, ushoroba wa Nchi ya Utukufu, kuangalia Hilo. Ninyi mnaoyaandika Maandiko, kwa kuwa ninawaona mkiandika, Timotheo wa Kwanza 3:16. “Bila shaka siri ya utauwa ni kuu: maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaaminiwa ulimwenguni, akaonekana na Malaika.” Malaika walisimama kumtazama Mungu. Wakati mmoja walikuwa wamezitikisa fimbo zao rasmi mbele Zake, wakilia, “mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,” wakati alipokuwa ameketi Pale,

kama Nguzo ya Moto, katika utukufu wa Mbinguni. Ndipo alipofanyika mtu, Malaika walikuja wakamtazama wapate kumwona, Yehova, aliyefanyika mwili. Hakika, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu."

91 "Nitawapa ishara ya milele," kwa kuwa Mungu alifanyika mwili miongoni mwetu. Aliishi katika mwili. Itakuwa ni ishara ya milele. Sio tu kwa wachungaji kuangalia na kuamini, bali kwenu nyinyi Maskani ya Branham, na kwa ulimwengu huu katili, kuamini ya kwamba huyo ni Mungu. Mungu alitoa hiyo ishara. Yesu alisema, "Kama vile Baba aliye hai alivyonituma Mimi, na akaja pamoja Nami, na alikuwa ndani Yangu; ndivyo ninavyowatuma ninyi, Baba aliye hai aende pamoja nanyi na awe ndani yenu, ishara ya milele. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Tazama, nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Nitakuwa pamoja nanyi. Mwisho wa ulimwengu, nitakuwa hapo pamoja nanyi."

92 Mtu fulani, kama nilivyosema hapo awali, anataka kumfanya Mungu mdogo, mfupi. Yeye alikuwa ni mwanadamu; Mungu alikuwa akimtumia mwanadamu. Mungu alikuwa akitumia mwili alioumba, Mwenyewe, kusudi apate kuumba kupitia Kwake, "Na kuwaleta kupitia Kwake wana wengi," yanasema Maandiko, "kupitia kwa huyo Mwana mtiifu. Kupitia mwana mmoja, wote walianguka. Kupitia Mwana mtiifu, wote wataishi, wanaoamini."

"Mungu pamoja nasi," ishara, kasema hiyo ingekuwa ndiyo ishara. Yeye alipenda sana kujirejelea Mwenyewe kama "Mwana wa Adamu," mtu Mwenyewe, mtu tu. "Mimi si kitu; Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe." Lakini ni Baba aliyekuwa ndani Yake, Imanueli, Mungu.

93 Yu—yule mtoto mchanga, Mungu, Yehova Mungu. Mtoto huyo mchanga aliyelia, huyo alikuwa ni Yehova. Mnaweza kuliona? Mungu akiishi ndani ya mtoto mchanga.

94 Mungu akiishi ndani ya tineja. Alikuwa ni tineja wa aina gani? Aliweka mfano. Wakati alipopotezwa na baba Yake na mama Yake, walitafuta kote wampate, nao wakamkuta hekaluni. Yeye alisema nini, kama tineja? "Hamjui? Hamjui kwamba sina budi kufanya kazi ya Baba Yangu?" Mfano kwa matineja.

95 Kama mwanamume, pamoja na madoido yote ya ulimwengu aliyopewa, kila kitu kikiwa moja kwa moja mikononi Mwake, kuwa mkuu sana kuliko watu wote, tajiri sana kuliko watu wote; Yule aliyeweza kuwaambia watu mahali samaki walikuwa na sarafu kinywani mwao, angeweza kupampu maji yaliyo mazuri sana kutoka kwenye visima na kuyageuza kuwa divai, ambaye angebadilisha chochote alichotaka kubadilisha; ambaye angeweza kuchukua biskuti tano na kuwalisha watu elfu tano. Akiwa na nguvu mikononi Mwake apate kuwa mtu mkuu sana, lakini hata hivyo alichagua kuwa maskini. Hata hakuwa na

kaburi wakati alipokufa. Ilimbidi kuazima moja. "Imanueli, hii itakuwa ndiyo ishara." Mungu anakujaje? Katika walio maskini. Mungu hufanya kazi namna gani? Itakuwa ni ishara ya milele, pamoja na maskini, wasio na elimu.

96 "Ishara," kasema yule nabii mke mkuu, Hana, wakati Simeoni alipoinua mikono yake hekaluni, na kumshika Huyo mtoto mchanga katika nguo za kitoto. Hana anasema, "Ni ishara itakayonenewa vibaya, kwa ajili ya kuanguka kwa Israeli, bali kukusanyika pamoja tena, pia, Nuru kwa Mataifa."

97 Ati nini? "Mungu pamoja nasi," sio katika walio matajiri na wenye kiburi, bali katika walio maskini. Alizaliwa katika zizi, "Mungu pamoja nasi." Yeye alifanya mambo ya namna gani? Angalieni mambo Yake aliyosema. Mwangalieni, yale aliyosema.

98 Kwa kuwa, Mungu Mwenyewe alisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni. Huyu ni Mwanangu ninayependezwa kukaa ndani Yake. Msikieni." Akasema, "Nitakuwa pamoja nanyi daima, hata mwisho."

99 Aliwatuma mitume Wake. Waliitia dunia moto, katika siku zao, Mungu akiwa mmoja na mwanadamu. Walibatiza watu katika Jina la Mungu huyo, Yesu Kristo. Waliishi karibu sana Naye hata akajidhihirisha Mwenyewe kupitia kwao, kupitia kwa ishara na maajabu na karama za Roho Mtakatifu. "Mungu pamoja nasi." Walihubiri kulikuwako na Mungu mmoja wa kweli aliye hai.

100 Mwanadamu amejenga kila namna ya minara juu ya miungu watatu au wanne, ama miungu wawili, bali kunaye Mungu mmoja. Ujumbe huo ulikuwa ufufuliwe katika siku za mwisho.

101 Afadhali muamshe mawazo yenu sasa, ifungueni mioyo yenu. Ombeni Mungu awafunulie hili, yale ninayojiandaa kusema.

Wakati Yeye alipokuja, alitimiza yale aliyosema nabii.

102 Na wakati anapokuja katika siku za mwisho, katika mvua za vuli za Mungu, wakati mvua ya masika na ya vuli pia zitakapomwagwa, Yeye yuaja jinsi hasa ilivyotabiriwa juu Yake. "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Kitu gani kilipaswa kutukia? Imanueli, Mwana yule yule, Nuru ile ile, Mungu yule yule aliyekuja kuishi katika mwili, pamoja na watu Wake kwenye Siku ya Pentekoste, atakuja vivyo hivyo katika siku za mwisho, kwa kuwa itakuwa ni Nuru ya jioni. Ni kitu gani? Kutakuwako na ishara, ishara ya milele: Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu, Mungu kupitia sisi. Mwanadamu na Mungu wanakuwa mmoja. Yesu alikufa, hata akatoa ule uhai wa thamani, kwenye uamuzi Wake. (Katika Ujumbe wa Jumapili iliyopita.) Kwa sababu, Yeye aliutoa kwa ajili ya uamuzi, apate kuwaleta wana wengi kwa Mungu. Imanueli pamoja nasi. Watu wa Nuru ya jioni, ingewavutia.

103 Wakati Mungu alipotoa ile ishara, “Hii itakuwa ndiyo ishara. Mungu atakuwa anaishi katika mwili.” Alifikiri hilo lingewavutia watu. Liliwavutia. “Kwa kuwa wote waliompokea, aliwapa Uwezo wa kufanyika wana wa Mungu.”

104 Nalo linapaswa kuwavutia watu wa Nuru ya jioni wakati Nuru iyo hiyo ilipoonyesha. Mungu na Kristo ni mmoja. Petro alisema, “Na ijulikane kwenu, ya kwamba Mungu amemfanya Yesu yuyu huyu, Ambaye mlimsulubisha, Bwana na Kristo pia.” Ishara, itakayonenewa vibaya, bali Nuru za jioni ziko hapa.

105 Kama marehemu mhudumu wa Injili, wakati ujumbe wa kipentekoste ulipoanza kuanguka, hayati Dk. Haywood, kabla tu. . . Yeye, nadhani, hakuninii. . . Labda wakati alipokuwa katika upeo wake, siku moja wakati Roho alipomgusa. Alikuwa ni mshairi, mbali na kuwa mhubiri. Aliinyakua kalamu yake na kuliandika.

Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Mapito ya utukufuni hakika mtayapata;
Katika njia ya maji ndiko kwenye Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubieni dhambi yenu yote,
Na Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Kwa kuwa Nuru za jioni zimekuja,
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni mmoja.

106 Nuru za jioni! Kama tunatembea katika Nuru ya jioni, ishara ya jioni, basi ilikuwa iwe ni Nuru ile ile na ishara ile ile, ishara ya Milele. Basi ishara zile zile zitaifuata Nuru ya jioni. Whiu! Mnaliona? Mnaweza kulielewa? Huo ndio Ujumbe Krismasi hii. Nuru za jioni, ishara za Masihi zikiambatana Nao, zikiambatana na Ujumbe. Nuru za jioni ziko hapa.

107 Unanenewa vibaya. Watakukataa, ndugu zako. Ni nani waliomkataa? Ndugu zake. Walipenda kumwona akifanya miujiza. Lakini ilipofikia Kalvari, wote walikuwa wapi? Inapofikia wakati huo muhimu, ambapo Mungu katika Ukweli Wake na Biblia Yake atadhihirishwa, wako wapi? Wanarudi nyuma.

108 “Kutakuwako na ishara mtakayopewa. Na ishara hizi zitafuata. Kazi nifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya; hata nyingi kuliko hizi, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu.”

109 “Itakuwa Nuru tena wakati wa jioni.” Loo, siku hii yenye giza ambayo tumepitia! Lakini kwa muda wa miaka arobaini mawingu yamekuwa yakiondoka, kupitia kwa yale matengenezo ya kwanza, ya kuuleta Ujumbe kwamba Mungu na Kristo ni mmoja, kwamba Mungu alidhihirika katika mwili. Alichagua kuishi katika mwili wa mwanadamu. Na leo hii wanamfanya kitu kilichoketi juu ya kiti cha enzi, wanamfanya kitu fulani cha zamani za kale, baadhi yao wanataka kumrudisha kwa mwanafalsafa, wengine wanataka kumfanya nabii. Lakini,

ndugu, Yeye ni Mungu ndani yako, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Vipi?

110 Walijuaje Yeye alikuwa Mungu katika mwili? Yeye alisema, "Nisipofanya kazi za Baba Yangu, basi nimewaambia uwongo. Lakini nikizifanya kazi za Baba Yangu, ninyi amininі."

111 Na sasa jambo lile lile. Ujumbe umefufuliwa tena katika siku za mwisho, Ujumbe wa kwamba Yeye ni Nani, kile alicho. Imanueli akiishi ndani yenu, pamoja na kazi zile zile alizofanya, akijidhihirisha Mwenyewe kupitia kwenu, mambo yale yale aliyofanya. Ni Nuru ya jioni. Inanenewa vibaya. Ni njia ngumu.

112 Ilimaanisha jambo fulani kwa yule kijana tajiri mtawala, hata hivyo moyo wake ulikuwa na njaa, kuja kwa Yesu, na kusema, "Rabi, nifanye nini nipate Uzima wa Milele?"

Kasema, "Zishike Amri."

Akasema, "Nimefanya hivyo tangu utotoni."

Kasema, "Unataka kuwa mkamilifu basi?" Kasema, "Unifuate Mimi."

113 Lakini aliondoka amehuzunika. Ilikuwa ni gharama kubwa kupita kiasi. Kama angaliweza kumpa Yeye pesa na kujenga kanisa kubwa mahali fulani, ajifanye mfuasi, angalifanya hivyo kwa urahisi. Hivi hamwoni vile hilo limefuata mtindo siku hizi miongoni mwa matajiri? Kulikuwako na wengine.

114 Sio tu matajiri, bali maskini; wengi wao kutoka kwenye mashimo ya vinamasi, na kadhalika, walikataa kwa sababu ya umaarufu. Kwa sababu, hakuwa maarufu. Yeye alikuwa Imanueli. Wao walisema, "Huo ni ukosoaji. Huyo—huyo ni ibilisi. Hiyo ni telepathia ya akili. Huyo—huyo ni Beelizebuli." Waalimu wa siku hizo, makanisa yao makubwa, yalisema, "Upuuzi."

115 Lakini Mungu alisema, "Ni ishara ya Milele, ishara kuu, ishara ya ishara zote, kwamba Mungu yuko pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu." Hiyo hapo ishara yenu kuu. Inashinda ishara zote. Ndiyo ishara ya kwanza. Matendo 19, ilibidi watu hao warudi na kuitambua ishara hiyo, kabla hawajaweza kumpokea Roho Mtakatifu, Matendo 19:5. Hata hivyo, mwaminio aliyekuwa na Biblia, na alikuwa na mhubiri mzuri ambaye alikuwa akithibitisha kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo, hata hivyo kabla hawajaingia ndani Yake . . . Na kuona ile ishara, ilibidi waje na kubatizwa tena, wawekewe mikono na kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

116 Lakini katika wakati wa Jioni, zile Nuru ziko hapa. Nazo zinakosolewa. Zinadhihakiwa. Zinanenewa vibaya. Nabii alisema zitanenewa vibaya, "Jiwe la kujikwaa." Kunenwa vibaya, kudhihakiwa, kukosolewa; Imanueli ndani yetu, akitenda mapenzi Yake kupitia sisi.

117 Loo, siku hizi, ndugu yangu msafiri, dada yangu, iamini ishara hiyo. Angalia katika hori la moyo wako mwenyewe,

uone kama unaweza kusema ndani yako. Itazame ile ishara ambayo wale wachungaji waliona. Mungu katika mwili, akiishi miongoni mwa maskini, wahitaji, waliotupwa nje. Uone kama unaweza kulifahamu. Mungu ndani ya moyo wako, Mungu *hapa* ndani. Angalia uone kama Yeye hujidhihirisha Mwenyewe vizuri, katika utamu na upole, kama alivyofanya.

118 Miaka michache iliyopita, kulikuwako na msichana aliyetoka akaenda chuoni, na, pamoja na wenzake wengi kule, akawa maskini mjuaji sana, kutoka kwenye mafundisho yake ya mashambani aliyokuwa amepata, kama mama katika nyumba ya mashambani. Basi siku moja akaamua, miaka miwili baadaye, kumtembelea mama yake tena. Akamwandikia barua ya simu na kumwambia ya kwamba angefika kwa garimoshi fulani, akamlaki kwenye stesheni. Walakini, alikuja na maskini mjuaji mwingine. Naye alikuwa amekuwa mjuaji, yeye mwenyewe. Basi akaja pamoja na mwingine, ambaye kidogo alikuwa ni mstaarabu mamboleo, kimbelembele, tineja.

119 Basi alipofika kwenye hiyo stesheni, alipoanza kutoka kwenye garimoshi, aliangalia. Basi pale alisimama mama yake, akiangalia kwa yote yaliyokuwa ndani yake, aone mahali bintiye alipokuwa. Ndipo wakati yule msichana aliyekuwa pamoja naye, mama. . . alipomwona huku uso wake umejaa makovu, na mikono yake imechomeka yote. Naye alionekana wa kutisha sana, mkongwe, na alionekana mbaya sana. Ndipo huyo msichana aliyekuwa na huyo Mary mdogo, akamwambia, "Nashangaa kile kizee kinachoonekana kibaya hivi ni nani?"

120 Basi huyo msichana akamwonea mama yake aibu. Akasema, "Sijui mimi. Sijui ni nani."

121 Naye mama yake, wakati alipomwona bintiye, alimkimbilia na kumkumbatia, akaanza kumbusu.

122 Akamsukuma, akasema, "Sikujui mimi. Umempata mtu mwingine," kwa sababu hakutaka kuhusishwa na mtu kama huyo ambaye mtu mwingine angemcheka na kumdhihaki.

123 Ikawa palikuwapo na mtu, kondakta wa garimoshi, amesimama karibu. Mara akamshika msichana huyo kwenye bega. Akasema, "Huna aibu, ewe mtu mwenye mashaka! Ninakumbuka kisa hicho vizuri sana."

124 Ndipo watu wakakusanyika kusikia yaliyokuwa yametukia. Naye akamshika huyo msichana vizuri sana, na akasema, "Msichana huyu mdogo, wakati hakuwa na umri wa miezi sita, alikuwa kwenye kitanda chake kidogo kwenye orofa ya juu. Naye mama yake wa thamani, mwanamke mrembo kuliko wote niliyepata kumwona," akasema maskini huyo kondakta. Akasema, "Nyumba ilishika moto wakati mama yake alipokuwa akianika nguo. Nao majirani wote wakakimbia, wakipiga mayowe. Waliuona. Mama kamwe hakuuona. Ulikuwa kwenye

upande wa baraza la hiyo nyumba. Nazo ndimi za moto zilikuwa zimeshika kabisa, nazo zilikuwa zimeenda hewani."

125 Kisha kasema, "Wasingeweza kumzuia huyo mama aliyeingia wazimu. Mtoto wake alikuwa kwenye orofa ya juu." Kisha kasema, "Wote walilia, 'Huwezi kupenya hiyo—hiyo miale ya moto.' Lakini yeye alinyakua shuka lililokuwa mkononi mwake, kutokana na kuyaanika, nalo lilikuwa shuka lililolowa maji. Ndipo akajifunika hilo, naye huyo akazipenya hizo ndimi za moto, na kwenye orofa ya juu, pasipo kufikiria juu ya hatari yake mwenyewe. Ndipo alipofika kule, alijua asingeweza kujifunika hilo shuka akirudi. Lakini, kuuokoa urembo wa bintiye uliokuwa umfuate, alimfunika huyo mtoto mchanga kwenye hilo shuka, kisha akapenya mbio kwenye hiyo miale, huku uso wake na mikono na vitengele vyake vikiwa wazi. Basi ukachoma nyama kutoka mwilini mwake, na kuyasinyaisha mashavu yake kwenye mifupa yake, na kumharibu sura, ukazichoma nywele zake zote, na ninii—ninii . . . mifupa yote kwenye kidole chake."

126 Kasema, "Akawa na sura mbaya, ili uweze kuwa mrembo. Aliupoteza urembo wake, alipoteza kila kitu alichokuwa nacho, ili aweze kukuokoa. Halafu ati unasimama na kumwonea aibu mama huyo wa thamani?"

127 Ndugu, ninapomwona Mungu, Mungu wa Mbinguni, alivyokiacha kiti Chake cha enzi, uzuri Wake, na yote aliyokuwa; apate kuzaliwa juu ya lundo la samadi, afunikwe nguo za kitoto, adhihakiwe kwa ishara Zake na maajabu Yake, aitwe ibilisi; je, ati nimwonee aibu? La, bwana. Acha huu ulimwengu maarufu ufanye yale wanayotaka kufanya. Kwangu mimi, Yeye ni ishara kuu. Roho Mtakatifu ndani yangu anapaza sauti. Huenda akanifanya nitende kiajabu na niwe mwenye kichaa, kwa ulimwengu huu, bali siwezi kumkataa Yeye Yule aliyenifanyia mengi sana. Alipachukua mahali pangu katika mauti. Alipachukua mahali pangu pale Kalvari. Alifanya mambo haya yote. Alijidhili kutoka Mbinguni, kutoka kwenye viti vyeupe vya enzi vya lulu, ili kuwa mwanadamu; apate kuonja mateso yangu, kupitia kwenye majaribu yangu, kujua jinsi ya kuwa mpatanishi anayefaa ndani yangu, kuniongoza na kunielekeza kwenye Uzima wa Milele. Na kupitia kwenye umaskini Wake, ninafanywa tajiri. Kupitia mauti Yake, ninapewa Uzima, Uzima wa Milele.

128 Usimkatae. Usimwonee aibu. Usimwonee aibu. Lakini mkumbatie, na kusema, "Naam, Mpendwa Bwana wangu, nipe kama walivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, Bwana. Nipe Roho Mtakatifu. Mmwage moyoni mwangu. Sijali matineja wanasema nini. Sijali walimwengu wanasema nini. Siwaangalii wao. Ninakuangalia Wewe." Ni kitu gani? Kujiunga na kanisa? La. Ishara kuu, Imanueli, Mungu pamoja nasi.

Na tuombe.

129 Kwenye kusanyiko la watu asubuhi ya leo, kuna wengine hapa ambao wangetaka kusema, "Kwangu mimi, ninayaonea aibu maisha yangu. Simwonei Yeye aibu. Ninayaonea aibu maisha yangu," kumtolea Yeye Ambaye alifanywa sura mbaya, na kudharauliwa na ulimwengu?

130 "Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko. Sote tulimficha nyuso zetu" alisema nabii. "Alidharauliwa na kukataliwa. Hata hivyo, tulimdhania amechapwa na kupigwa na Mungu. Hata hivyo, alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tulipona."

131 Waweza kumwonea aibu? Kama unaweza, njoo madhabahuni ukatubu dhambi yako. Endapo humwonei aibu, na unayaonea aibu maisha yako ambayo ulimkabidhi, kitu kibaya hivyo. Umeona aibu mara nyingi, mbele ya bosi; mbele ya rafiki yako wanawake, mbele ya rafiki yako mwanamume, mbele ya rafiki yako msichana ama rafiki mvulana. Umemwonea aibu, Imanueli akiishi ndani yako. Inua mkono wako na useme, "Mungu, nisamehe kwa kuona aibu."

132 Bwana wetu na Mungu wetu, kwa unyenyekevu na kwa hisani kubwa tunakuomba utuwie radhi, asubuhi ya leo, kwa kupungukiwa kwetu kwote, kwa kuwa sisi sote mara nyingine tuna hatia. Tuna hatia ya kuitetea Kweli. Tuna hatia. Wanapotaka kutuita jina ovu, kama, loo, "mtakatifu anayejibingirisha," ama kitu kiovu kisicho, hata hivyo wakati mwingine tunarudi nyuma kama Petro na kujipasha moto kwenye moto wa adui. Tusamehe, Bwana.

133 Mwaka mpya unatukaribia. Jalia tuanzie kwenye saa ii hii, na tuione ile ishara kuu ya Mungu miongoni mwetu, Mungu akiishi pamoja nasi, akiishi ndani yetu, akitenda, akifanya jinsi alivyofanya hasa. Nazo Nuru za jioni ziko hapa.

Tusamehe kupungukiwa kwetu. Tusamehe dhambi zetu.

134 Nasi kwa hisani sana, Bwana, tunaikubali Zawadi Yako ya Krismasi, Mwana wa Mungu, kuishi mwilini mwetu, mavumbi yetu, kuishi pamoja nasi, akiitakasa njia Yake kwa Damu Yake Mwenyewe, na kutupa hakikisho la Uzima wa Milele. Tunakushukuru Wewe. Ninakushukuru Wewe, Bwana, kwa ajili ya Uwepo huu mkuu wa ajabu kutoka kwa Mungu, kwa kuwa ni zawadi, zawadi ya Roho Mtakatifu iliyofungwa katika Jina la Bwana Yesu. Tunafurahia kuipokea. Tunakushukuru Wewe kwa sababu kanisa letu linaitetea ishara hiyo, kwa sababu hiyo ishara inasimamia Fundisho la Kanisa. Tunaitetea. Inatutetea. Pia inajulikana miongoni mwa Wakristo kote ulimwenguni leo hii, kuhusu maskini kundi la watu wasio na elimu, kwenye Barabara ya 8 na ya Penn, huku Jeffersonville; ya kwamba Imanueli, ile Nguzo ya Moto kutoka nyikani, yule Yesu wa

Galilaya, Roho Mtakatifu wa Pentekoste, amedhihirishwa na ishara zote za Imanueli katika Nuru za jioni. Tunashukuru sana, Bwana. Basi jalia wengine waione na kuipokea. Kwa kuwa, tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake na kwa ajili ya Kanisa. Amina.

135 Laiti ningalikuwa na sauti ya mwimbaji. Kama ningalikuwa na sauti ya mwimbaji sasa hivi, ningependa kuwaimbia wimbo ninaoupenda sana, ulioandikwa na rafiki yangu wa thamani, William Booth-Clibborn.

> Alishuka kutoka utukufuni Mwake, ndiyo hadithi iishiyo daima,
> Mungu na Mwokozi wangu alikuja, nalo Jina Lake lilikuwa ni Yesu.
> Alizaliwa horini, kwa walio Wake akawa mgeni,
> Mungu wa huzuni, machozi na uchungu mkali.
>
> Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomwabudu!
> Uzima wangu, mwanga wangu wa jua, yote katika yote kwangu!
> Yule Muumbaji mkuu akawa Mwokozi wangu,
> Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.
>
> Ni kujidhili kwa namna gani, akituletea ukombozi;
> Wakati katika usiku wa manane, pasipo na wakia wa tumaini ulioonekana; (Ndipo ikaja radi iliyogawanyika!)
> Mungu, wa thamani, mpole, aliweka kando utukufu Wake,

Akajidhili kwenye hori, zizi lililojaa samadi, apate kuzaliwa mle ndani.

> Akijidhili apate kuibembeleza, kuishawishi na kuiokoa nafsi yangu.
>
> Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomwabudu!
> Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote katika yote kwangu!
> Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
> Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

136 Halafu Yeye yuko ndani yangu, nami niko ndani Yake. Na ndani yako . . . "Katika siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu," Mungu, Imanueli, pamoja nasi.

137 Ilikuwa ni Imanueli huyo aliyemwona George Wright, anayeketi pale sasa hivi; amelala pale akifa, wakati madaktari wanne walipompita. Ilikuwa ni huyo Imanueli, ilipomlazimu kuazima tumbo la uzazi, ilipomlazimu kuazima ka—kaburi. Yeye aliazima macho yangu, kasema, "Nenda kamwambie Ndugu George, 'BWANA ASEMA HIVI. Yeye atachimba kaburi la wale wahubiri na kadhalika wanaomcheka.'"

138 Ilikuwa ni huyo Imanueli. Ilikuwa ni Yuyo huyo, kuhusu wale wanyama wadogo, hivi majuzi mwituni. Ilikuwa ni Yuyo huyo, kuhusu Margie Morgan anayeketi pale, hao wengine wote. Ilikuwa ni Yuyo huyo ambaye aliazima welekevu wa akili, hisi za mwili, kujiwasilisha Mwenyewe kwa ulimwengu siku hizi, kupitia wewe, wakati Nuru za jioni zikiwaka. Mungu aturehemu, rafiki.

139 Ninachukua muda wenu mwingi sana. Hebu tuujaribu. Tupe sauti, "Loo jinsi ninavyompenda!" Ni wangapi wanaoujua?

> Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomwabudu!
> Uzima wangu, mwanga wangu wa jua, yote katika yote kwangu!
> Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
> Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Kushuka Kutoka Utukufuni Mwake*—Mh.]

> Jinsi ninavyomwabudu!
> Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote katika yote kwangu!
> Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
> Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

140 Sasa ni wakati Wake wa kutuonyesha neema Yake. Mama anamleta mtoto wake mchanga hapa, mwenye lukemia, kansa kwenye mkondo wake wa damu. Uovu huo kwa mtoto mchanga?

Mungu, hii hapa sauti yangu; nena Neno, nalo litatimia.

Kwa kuwa, Bwana, Wewe ulisema, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka.' Usitie shaka. Litatimia."

Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninamhukumu ibilisi huyu anayeitwa lukemia. Ugonjwa wa mwili wa mtoto huyu, utaondoka. Hauna budi kumwacha. Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo.

Mwanga wangu wa jua, yote kwa yote kwangu!
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

141 Jinsi ninavyompenda! Kamwe siwezi kumwachilia. Ninataka, kama Yakobo, kumshikilia.

. . .mwabudu!
Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote katika yote kwangu!

"Hii itakuwa ishara."

Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

142 Yeye si ni wa ajabu? Hivi hamjisikii tu kumwabudu? Katika Roho tu, mwabuduni tu. Jisahau tu sasa. Usione haya. Roho Mtakatifu yuko hapa. Huyo ni Roho Mtakatifu. Kwa unyenyekevu tu, kwa njia yako mwenyewe.

Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

Haya basi.

Ni kujidhili kwa jinsi gani, kunakotuletea ukombozi; ("Itakuwa ishara.")
Ambapo katika usiku wa manane, hapakuonekana hata na tumaini moja dogo kabisa;
Mungu, wa thamani, mpole, aliweka kando fahari Yake, (Wazieni yale aliyofanya!)
Akijidhili kuibembeleza, kuipata na kuiokoa nafsi yangu.

143 Na tuinue mikono yetu tunapouimba.

Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomwabudu!
Pumzi yangu, mwangaza wangu wa jua, yote katika yote kwangu!
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

144 Bwana, kamwe hatutafahamu utajiri, utimilifu wa Roho Yako, mpaka tutakapomwona kwenye siku ile wakati atakapokuja. Huenda tukalala mavumbini. Huenda ikanilazimu kurudi kwenye mavumbi asili, bali hilo halitanihangaisha

hata kidogo. "Ninajua ya kwamba Yeye ataita, nami nitajibu. Na ndipo nitamwona jinsi alivyo. Mwili huu uharibikao utabadilishwa na kufanywa kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambapo Yeye anaweza kuvitiisha vitu vyote Kwake."

145 Sikuzote nitakushukuru kwa ajili ya ile zawadi ya Krismasi ya Kristo moyoni mwangu, kujua ya kwamba ni Kristo yule yule, kwa sababu anafanya jambo lile lile. Linanifanya kujisikia na kutenda kama Yeye alivyofanya hapo mwanzo, kwa mtumishi Wake.

146 Ninashukuru kwa ajili ya kanisa la ulimwenguni kote, lililoshinda, tayari limekusudiwa tangu zamani, na kuitwa, na kutiwa muhuri, na kukusudiwa kwenye Mwili ule. Ninawapata katika Asia, Afrika, Urumi, kila mahali, Indiana, kupitia nchini, Afrika. Kila mahali kote ulimwenguni, ninaliona Kanisa hilo lililoshinda, ambao wanajua ya kwamba Wewe umekuja katika mwili. Nawe ulisema ya kwamba, "Kila roho . . . " Katika Biblia Yako, Wewe ulisema, "Kila roho isiyokiri hili, ni roho mbaya, mpinga Kristo. Kila roho isiyoshuhudia jambo lili hili, ya kwamba Kristo amekuja katika mwili wetu, ni roho ya mpinga Kristo."

147 Baba Mungu, nisaidie ku—kunyakua vikinga hivi vya moto huko ng'ambo. Ninaweza kuviona, Bwana, huko ng'ambo. Kuwaona wenye ukoma malangoni, kuangalia India huko ng'ambo, kwenye ile Taj, langoni, maskini watu hao wakitambaa sakafuni, hawana miguu. Kuwaona maskini wavulana hao wadogo huko ng'ambo katika Afrika, wakiinyosha juu maskini mikono yao. Ee Mungu, nitume mimi, Bwana. Jalia Malaika aje na kaa la Moto, achome ndani ya nafsi yangu, Bwana, na kutoa takataka zote na uvivu nje, nipate kwenda kama ki—kinga cha moto wa Mungu kuwanyakua kutoka motoni hao walio kwenye giza kuu.

148 Libariki kanisa langu dogo, Bwana. Loo, ninaweza kuona maskini mburuzo wa unga wa mbao kupitia hapa, na kuwaona hao watu wa thamani. Watu wakiendesha na kupita kwenye magari yao, wakiwacheka, kwa kuwa wameinua mikono yao, wakimsifu Mungu. Lakini siku moja Yesu atakuja, na mambo yote yatafanywa sawa. Hatutaaibika, Bwana. Tutaungana na Paulo wa kale, na kusema, "Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni Nguvu za Mungu kwa wokovu, kwa Uzima wa Milele, kwa kila mtu aaminiye." Tusaidie kuishi hivyo, Baba. Tunakuabudu sasa katika Roho, katika mahali pa Mbinguni. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kuzuriwa huku asubuhi ya leo. Katika Jina la Yesu. Amina.

149 Mara moja tu zaidi, sivyo?

Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ni- . . . (Bwana
Yesu . . . ? . . . katika Jina la Yesu.)

. . . yote katika yote kwangu!
Yule Muumba mkuu akafanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

150 Ninamtaka Yeye tu zaidi, nawe je, Doe? [Delores anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Huyo ni dada yangu, dada yangu kimwili.

Loo jinsi . . .

Binti mkwe wangu. Wanamtaka Mungu zaidi. Ndugu Grimsley anakuja, akimtaka Mungu zaidi.

Yote . . .

Hilo ndilo. Ndugu Wood, anakuja. Ndugu Collins, mhubiri Mmethodisti; mkewe, wengine.

. . . akafanyika Mwokozi wangu.

Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu, akiita, Mwenyewe.

. . . unakaa ndani Yake.

Loo jinsi ninavyopenda . . .

Lionyeshe tu kwa njia yako mwenyewe sasa.

Jinsi ninavyomwabudu!
Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote kwa yote kwangu!
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

151 Bwana, Bwana, hawa hapa, kondoo wa malisho Yako. Walishe, Bwana, kwa Roho Wako. Wanajitolea Kwako, Bwana. Wanayaweka wakfu maisha yao Kwako. Walisimama kwa sababu hawaoni haya kwa ajili ya Injili ya Yesu Kristo. Tunajua ya kwamba Wewe uko hapa, ile Nguzo kuu ya Moto, yule Kristo, Roho Mtakatifu.

. . . -mwabudu!
Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote kwa yote kwangu!
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

152 Nena tu katika maneno yako mwenyewe sasa. Huyo ni Roho Mtakatifu aliyekuleta hapa. Mwambie tu unampenda. Roho Mtakatifu yeye yule aliyewainua kwenye Pentekoste, mnasimama hapa mkilia, mkiomboleza, mkishangilia.

Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

Pasipo na kusitasita, mwili na damu kiini Chake, (maskini mtoto mchanga ndani yake)
Alichukua mfano wa mwanadamu, akaufunua mpango uliofichwa.
Loo siri yenye utukufu, Dhabihu ya Kalvari,
Na sasa najua Wewe ndiwe yule "MIMI NIKO" aliye mkuu.

Loo jinsi mimi...Ee Mungu! Jinsi ninavyomwabudu!
Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote kwa yote kwangu!
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

153 Loo upendo ambao hautaniruhusu kwenda, upendo unaoshika moyo wangu zaidi ya chochote, utamu wa Uwepo wa Roho Mtakatifu; wakati kanisa Lake linaposimama karibu na madhabahu, likimwabudu, likiangalia zizini, likiona kitu kile kile mamajusi walichoona, Mungu aliyefanyika mwili.

...alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

154 Kukiweko na kasoro yoyote maishani mwako, ikiri sasa katika Uwepo wa Roho Mtakatifu, wakati kwa utulivu. Tazama moyoni mwako, uone kama kuna zizi mle linaloweza kustahimili ukosoaji, juu ya maungamo yako kwamba Yeye ni Mungu.

Utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

155 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, omba tu, wewe mwenyewe. Hii ni Roho Mtakatifu. Hivi hamwezi kuhisi unyenyekevu na upole wa Roho wa Mungu, utamu, Uzima udumuo?

156 "Zikiwapo lugha, zitakoma. Ukiwapo unabii, utabatilika. Yakiwapo maarifa, yatashindwa. Lakini upendo ujapo, unadumu milele." "Upendo huvumilia. Hautakabari. Haujivuni. Haukosi kuwa na adabu. Bali hutunyenyekeza, unatufanya watamu, unatia utamu nafsini mwako."

157 Na tuombe sasa, kila mmoja kwa njia yako mwenyewe, tukimshukuru Mungu kwa yale aliyofanya.

158 Ee Bwana, katika utamu wa wimbo huu, ukionyesha kwa ulinganifu wa sauti, sio sauti isiyojulikana, bali sauti inayomaanisha, kwetu, kwamba Mungu wetu ni nani, kama vile

Neno limelielezea. Sasa muziki unalielezea. Sasa mioyo yetu inalielezea, Bwana, mitazamo yetu Kwako. Tunakuja mbele. Wamesimama kwa miguu yao. Wanakupenda. Pamoja, Bwana, tunasimama kama kondoo Wako, kondoo wa malisho Yako. Tunakipenda Chakula hiki, ni kizuri kwa nafsi zetu. Nasi tunajua ya kwamba Mungu anaishi pamoja nasi. Tunajua ya kwamba Mungu alijimimina ndani ya Kristo, naye Kristo akajimimina ndani ya Kanisa.

159 Nasi hapa tunasimama leo hii, wakati kila namna ya dini, na kila namna ya—ya madhehebu na awamu, kila namna ya imani, bali hata hivyo Neno linajitetea Lenyewe, Mungu akidhihirishwa. Ile ishara kuu kwamba Mungu angali amedhirishwa katika mwili wa watu Wake, akifanya ishara zile zile na maajabu, akionekana katika mfano wa Wingu, Nguzo, akiishi miongoni mwetu, akiipambanua mioyo yetu, akitutabiria mambo yajayo, akiyaponya magonjwa yetu, akitufanya watu wanaoelekea Mbinguni sana hata tunajisahau. Mpaka, tunafanya mambo ya kigeni, kwa watoto wa ulimwenguni; jinsi wanavyosimama na kucheka, na kudhania ya kwamba sisi ni wendawazimu, kama tu walivyofanya kwenye Pentekoste, wakisema, "Hawa wote si wamelewa?"

Lakini jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomwabudu!
Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote kwa yote kwangu!
Yule Muumba mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.

160 Mnainua mikono yenu sasa kuahidi imani yenu kwa Mungu, nadhiri zenu kwa Mungu, uaminifu wenu na ukweli wenu kwa Mungu, kanisa lote?

161 Sasa sisi, Bwana, tunajikabidhi Kwako, baada ya baraka hii ya dhihirisho la Uwepo Wako, tukijua ya kwamba Mungu angali amedhihirishwa katika mwili wetu. Yeye alifanyika mavumbi yetu, alifanyika wa ukoo wetu; alijibadilisha kutoka Mungu akawa mwanadamu, mwanadamu apate kuishi ndani Yake. Nasi tulikuhisi Wewe asubuhi ya leo, katika roho zetu. Tunaziona kazi Zako na madhihirisho Yako. Tunakupenda. Tunajidhamini upya Kwako: kukuheshimu, kukupenda, na kufanya kila kitu tujuacho jinsi ya kufanya, ambacho kingekuwa cha kupendeza, kuishi maisha ambayo yangekuwa kama Wakristo, ambayo hayangeleta lawama, bali yangekuwa ni baraka kwa Jina Lako kuu Takatifu. Haya tunafanya, Bwana, kama watoto Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

162 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani kabla hamjaketi chini. Ninyi kamwe mlipata kuhisi kitu kitamu hivi? Ule utamu wa

Roho Mtakatifu! Hakuna mtu wa kusema neno; ni kusimama tu moja kwa moja, kuja mbele. Utukufu wa Mungu! Mnaona?

163 Nimekuwa nikiomba na kusoma, siku mbili, juu ya hili. Zaidi ya hizo. Tangu Jumapili iliyopita, ama iliyopita, naam, Jumapili.

164 Jinsi ambavyo Ishara hiyo kuu, jinsi ambavyo Mungu alisema, "Nitawapa ishara. Nitakuwa mwilini mwao. Nitakuwa kama wao; watakuwa kama Mimi." Alisema Malaika wanaangalia. Ama alisema . . . Malaika waliwaambia wale wachungaji, "Angalieni zizini, mtaona kile ninachomaanisha." Ishara hiyo haikuwa ni kwa Malaika tu. Haikuwa ni kwa wachungaji tu. Ni kwa ajili ya ulimwengu, kuona na kuamini ya kwamba Mungu anaishi katika mwili.

165 Na kupitia kwa kutolewa kwa mwili huo, Yeye aliutakasa mwili wetu, apate kuishi ndani yetu. Mungu ndani yako. Kristo ndani yako. "Tazama, niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari." Msisahau hili. Liwekeni mioyoni mwenu.

166 Nilipokea baadhi ya zawadi nzuri sana za Krismasi, kamera ya sinema, na vitu vingine vingi, bunduki na kadhalika, kwamba watu wananipenda, walinipa. Jinsi ninavyothamini hilo!

167 Lakini, loo, huu, Uzima huu wa Milele, lile hakikisho lililobarikiwa ya kwamba Kristo anaishi ndani yetu, ya kwamba utimilifu Wake unaishi ndani yetu, unatufanya kusimama na kutenda tofauti. Kwa sababu, wewe, unapofanya hivyo, unakuwa mkimbizi kwa mambo ya ulimwengu. Unakuwa msafiri. Unajihesabu umekufa kwa mambo ya ulimwengu, na u hai katika maisha mapya. Sasa wewe ni mgeni ulimwenguni. Wewe ni mgeni kwa sababu umekiri hadharani, kwa matendo yako, kwamba, "Kuna Mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu." Mnaona? Nawe huyajali tena mambo haya ya ulimwengu, lakini sisi ni watu wanaoelekea Mbinguni tukiutazamia Mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni . . . wa Mungu. Sisi ni Uzao wa Ibrahimu kwa sababu tumemwamini Bwana Yesu Kristo, nasi tumekufa kwa mambo ya ulimwengu, na tumefufuliwa tena katika ufufuo wa sura Yake; tupate kutembea kama alivyofanya Ibrahimu, akiutafuta Mji ujao, akilichukua Neno la Mungu, akiita kingine chochote kwamba ni kinyume, kuwakaribisha Malaika nyumbani mwetu, kama alivyofanya Ibrahimu, wale wajumbe wa Mungu, waliouleta ujumbe. Loo, ni wakati wa jinsi gani! Tukikiri ya kwamba hatuutaki ulimwengu tena. Tunamtaka Yeye, na Yeye pekee. Yeye ndiye Mwokozi wetu.

168 Unaposafiri kutoka kwenye jengo hili asubuhi ya leo, nenda pamoja Naye. Kamwe usimwache aondoke. Kuwa mtamu nafsini mwako, siku zote za maisha yako. Mungu awabariki sasa mnapoenda kwenye viti vyenu, nao watoto wanapokea zawadi zao. Mungu awabariki.

169 Ni wa kuombewa? Wasaidie wapitie hapa, dada. Wataomba wafanikiwe.

Bwana Mungu amrehemu ndugu huyu. Mwondolee roho ya ulevi, Bwana. Jalia alewe kwa Divai mpya ya Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

170 Hii si ni ya Kimbinguni tu? Ni wangapi wanaojisikia hivyo, huu tu, utamu tu? Hakuna mtu ajuaye la kusema. Sijui lolote la kusema. Ninaninii tu—nina . . . nimekosa maneno. Si—sijui la kusema. Roho Wake ameingia tu ndani, mnaona.

171 Ni kitu gani? Mnakuwa wana-kondoo, naye Hua yuko hapa kuwaongoza kwenye Chakula cha mwana-kondoo, Chakula cha kondoo. *Hiki* ni Chakula cha kondoo, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu." Roho zetu huishi kwa Hicho.

172 Nafikiri sasa ninapaswa kumwona rafiki yangu mzuri, Attorney Robinson, laiti ungengojea tu kwenye hili jengo muda mrefu kutosha mpaka ninapoweza kubadilisha nguo zangu, nirudi, maana nimelowa jasho.

173 Ndugu Neville ataichukua ibada sasa, kwa ajili—kwa ajili ya zawadi za watoto. Bwana awabariki.

174 Sikuzote imbeni *Alishuka Kutoka Utukufuni Mwake*. Mnapofanya hivyo, kumbukeni kile tunachoamini katika Yeye, "Utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake."

Mungu akubariki, Ndugu Neville.

175 [Ndugu Neville anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Naam, ukitaka nifanye hivyo. ["Naam."]

176 Ndugu Neville aliniuliza kama ningerudi usiku wa leo, tena, kuhubiri usiku wa leo tena. Ninachukia kuchukua ibada yake. Lakini niko hapa, hiyo ndiyo sababu ya mimi kuwa hapa. Sawa, nitarudi usiku wa leo, Bwana akipenda, kuzungumza kwenye ibada.

*Ishara Kuu* SWA59-1227M
(A Super Sign)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 27 Desemba, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org